# *Uanafunzi: Kumfuata Yesu*

THOMAS GOLDING

AUTHENTICITY
BOOK HOUSE
in partnership with
twelve21
GLOBAL

*Uanafunzi: Kumfuata Yesu*

Hakimiliki © 2021 na Thomas Golding

Wahariri: Erin Ensinger, Fran Geiger Joslin, na Dianne L. Taylor

ISBN (4 x 6 English paperback): 13: 978-1-943004-42-3
ISBN (English eBook): 13: 978-1-943004-43-0
ISBN (4 x 6 Swahili paperback): ISBN: 978-1-943004-48-5
ISBN (Swahili eBook): ISBN: 978-1-943004-59-1

Authenticity Book House
Winterset, IA 50273
www.ABHBooks.com
abhinfo@abhbooks.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu yoyote ya uchapishaji huu inayoweza kuzalishwa tena, kutunzwa katika mfumo umbao unaweza kurejeshwa tena, ama kusambazwa kwa mtindo wowote au katika njia yoyote – kielektroniki, kiufundi, kinakala ya nakala (photocopy), kwa kurekodi au njia nyingine - isipokuwa kwa nukuu fupi katika mapitio yaliyochapishwa, pasipo ruhusa ya awali ya mchapishaji.

Maandiko yote yatatafsiriwa kutoka katika lugha ya awali ya muandishi, Thomas Golding, isipokuwa kama imeonyeshwa vinginevyo.

Nukuu za maandiko zinazotumika katika sehemu ya tafsiri ya kitabu cha "Good News for You (Habari Njema Kwako)" zitatolewa kutoka katika Biblia Takatifu, New International Version® (Tafsiri Mpya ya Kimataifa). Hakimiliki© 1973, 1978, 1984 na International Bible Society (Jamii ya Biblia ya Kimataifa). Inayotumika kwa ruhusa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa.

Kwa sababu ya asili ya mabadiliko ya mtandao, anwani yoyote ya wavuti (web address) au viungo vya wavuti (links) vilivyomo katika kitabu hiki vinaweza kuwa vimebadilika tangu vilipowekwa mtandaoni na vinaweza visitambulike tena.

Mtindo wa jalada: Schechner & Associates

Muundo: Ramesh Kumar Pitchai

AUTHENTICITY BOOK HOUSE in partnership with twelve21 GLOBAL

10 9 8 7 6 5 4 3 2 1
Imechapishwa na Authenticity Book House
Kutolewa United States of America (Marekani) na MiniBük

## Huduma ya Authenticity Book House

Authenticity Book House (ABH) hutoa **vijitabu vidogo kwa ajili ya mafunzo ya wachungaji.** Tunasambaza vitabu vyenye fundisho linalokubalika kitheolojia kwa wachungajia ambao wana mafunzo kidogo au hawana kabisa mafunzo ya kina ya Biblia. ABH hurahisisha Yaliyomo ili kufikia kiwango stahiki cha usomaji bila kupunguza uzito wa kweli muhimu zinazohitajika kwaajili ya mambo ya kiroho na uongozi.

Umbo dogo la vitabu vyetu hurahisisha usafirishaji na utoaji kwa bei nafuu. Kwakuwa vitabu hivi husafiri zaidi ya kile kituo cha kwanza kilicholengwa, tunaambatanisha ujumbe injili unaoeleweka, tukizisambaza habari njema kwa kadiri ya umbali ambao kitabu kitaenda.

Mfumo wetu wa utoaji wa vitabu ni wa ushirikiano wa kundi ambalo ni pamoja na wanatheolojia na waliothibitishwa wahariri, waandishi wabobevu na wafasiri, na washauri waelekezi juu ya tamaduni.ABH iv Kuhusu ABH inakusudia kutoa mtaala kamili kwaajili ya kuwajengea wachungaji uwezo. Tunatoa machapisho mengine pia ili kuwezesha huduma

yao kuwafikia maaminio wapya na washirika walio katika hali ya kurudi nyuma.

# Yaliyomo

## Contents


Utangulizi: Kitu Gani Mungu Anafanya Hapa Duniani? . . . . . 1
Uanafunzi: Mpango wa Mungu tangu Mwanzo . . . 1
Uanafunzi: Kuujaza Ulimwengu na Sura ya Mungu . . . . . 1
Nini Kiliutokea Mpango mzuri wa Mungu? . . . . . . 3
Yesu: Mfano Kamili wa Mungu . . . . . 6
Uanafunzi: Kuwa Kama Yesu . . . . . 8

Sura ya 1: Mwanaume Huyu ni Nani? Kumtambulisha Yesu (Marko 1:1–8:21) . . . . . 11
Masihi Aliyetiwa Nguvu na Roho (1:1-15) . . . . . . . 13
Masihi Astahiliye Kufuatwa (1:16-20) . . . . . 14
Masihi Mwenye Mamlaka na Nguvu (1:21-45) . . . 16
Masihi Mvunja Kanuni (2:1–3:6) . . . . . 17
Masihi Mtenda Miujiza (3:7–6:6) . . . . . 19
Masihi Abadilishaye Mioyo (6:7–8:21) . . . . . 22

Sura ya 2: Anafanya nini? Umisheni wa Yesu
(Marko 8:22–10:52) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .29
Kuanza Kuuona Umisheni (Marko 8:22-30) . . . . .30
Umisheni: Kuteseka Sasa,
Utukufu Baadaye (Marko 8:31–9:29). . . . . . . . .31
Umisheni: Kutumika kwa
Unyenyekevu (9:30–10:31) . . . . . . . . . . . . . . . . . .33
Umisheni: Kutumika kwa Kuacha
Kila Kitu (10:32-45) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .36
Kuuona Umisheni Wazi Zaidi (10:46-52). . . . . . . .37

Sura ya 3: Wanafunzi Hubakia Waaminifu kupitia
Mateso (Marko 11:1–16:8) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .43
Njia ya Mateso (11:1–13:37). . . . . . . . . . . . . . . . . . .43
Machaguo Mawili: Kujiokoa Mwenyewe au
Kujikana Mwenyewe (13:37-16:8). . . . . . . . . . . . .45
Yesu, Mwaminifu Pekee . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .48
Kumtegemea Aliye Mwaminfu. . . . . . . . . . . . . . . . .49

Sura ya 4: Ni nini Kifuatacho! Mawazo ya
Kivitendo kuhusu Uanafunzi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . .53
Onyo kwa Waongofu Wapya . . . . . . . . . . . . . . . . . .54
Kugundua Zaidi kuhusu Yesu na Maisha yake . . .58
Sala. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .61
Ushiriki wa Mikono. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .61
Muda na Uvumilivu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .65
We Ungefanya Nini? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .66

Hitimisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71

Habari Njema kwako . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 75
Jinsi ya Kukubali Zawadi ya Wokovu: . . . . . . . . . . . 77
Mfano wa Maombi ya Wokovu: . . . . . . . . . . . . . . . . 77

Maelezo ya mwisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 79

# Utangulizi

## Kitu Gani Mungu Anafanya Hapa Duniani?

**Uanafunzi: Mpango wa Mungu tangu Mwanzo**

Maneno ya kuagana ya Yesu alipokuwa akiondoka duniani yanabakia kuwa moja ya amri zake bora zilizojulikana: "Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi" (Mathayo 28:19). Lakini kufanya wanafunzi hakukuanza na Yesu. Kuanzia sura ya kwanza ya Biblia, Mungu anauonyesha moyo wake kwa kile tunachoita sasa uanafunzi. Kiurahisi, uanafunzi maana yake ni kumfuata Yesu, kufanyika mwanafunzi wa mwalimu mkamilifu tukijifunza njia za maisha yake.

**Uanafunzi: Kuujaza Ulimwengu na Sura ya Mungu**

Mwanzo kabisa wa uumbaji, dunia ilining'inia katikati ya hewa tupu "ikiwa tupu na pasipo umbo" donge la kitu lisilo na umbo na lenye utupu (Mwanzo 1:2). Kwa siku sita Mungu akafanya kazi ya kulipa donge hilo umbo na kulijaza, kulifanya liwe makazi sahihi kwaajili

ya wale ambao mwishoni angewaweka. Katika kila mwisho wa hizo siku sita, neno lilijirudia likisema, “na Mungu akaona ya kuwa ni chema” ikitoa ishara ya kuwa ndiyo mwisho wa kazi ya siku hiyo.

Mungu aliutangaza mwanga kuwa ni mwema kwa maana ulililiangazia giza. Akautangaza utenganisho wa nchi kavu na bahari kuwa kazi nyingine njema. Akaiita miema miti na mimea iliyochipua juu na kuijaza dunia. Jua, mwezi na nyota vilivyotawala usiku na mchana, viumbe vilivyoijaza bahari, ndege walioijaza anga, na wanyama wakiongezeka nchi kavu. Mungu aliyatangaza matendo yote ya uumbaji ya kuwa ni mema.

> Mungu aliiumba dunia kamilifu na kila kitu akakiweka mahali pake tayari kwa ajili ya kazi yake ya mwisho—wanadamu! Mungu akawaumba wanadamu, mwanaume na mwanake, *katika mfano wake mwenyewe*: Tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; atawale samaki wa baharini, ndege wa angani, wanyama wa kufugwa, dunia yote na viumbe vyote vitambaavyo. (Mwanzo 1:26)

Ni lazima Mungu atakuwa anataka tujue ya kuwa alituumba kwa mfano wake, kwamaana msitari wa 27 unairudia kauli hii mara ya pili! Mungu aliwabiriki wote mwanaume na mwanamke, akiwapa majukumu:

> Zaeni muongezeke, mkaijaze nchi na kuimiliki; muwatawale samaki wa baharini, ndege wa angani, na kila kiumbe hai kitembeacho duniani. (Mwanzo 1:26)

Mungu alipochukua hatua moja nyuma na kutazama yote aliyofanya, aliyatamka kuwa ni "mema" (Mwanzao 1:31). Ni picha iliyo nzuri ya ulimwengu! Ni dhahiri kabisa kuwa Mungu anataka kuwabariki wanadamu na kuwapa yaliyo mema. Anataka wautawale na kuutunza ulimwengu. Anawataka waujaze ulimwengu na sura yake mwenyewe, ikiwa na maana ya kuujaza ulimwengu na *watu wenye kumfanana Mungu*.

**Nini Kiliutokea Mpango mzuri wa Mungu?**

Ni dhahiri kuwa wanadamu wa kwanza hawakutunza amri za Mungu. Walipochagua kutenda dhambi, wakaharibu uumbaji

mkamilifu wa Mungu. Dhambi siyo tu kukiuka amri za Mungu. Kimsingi zaidi, tunapokaidi, tunaonyesha namna gani vile hatumuamini Mungu katika kutupatia yaliyo mema. Katika uumbaji, Mungu alitoa na kufafanua wema/chema ni nini, lakini hapo hapo akatokeza nyoka. Nyoka akatoa wazo la kwamba kuna kitu Mungu alikuwa anajaribu kuwaficha jambo jema Adamu na Hawa kwa sababu Mungu alitaka kuwatawala. Kwa mara ya kwanza, mwingine mbali na Mungu anatoa maana ya "wema/chema". Hawa akachukua tunda lililokatazwa na kulila, akimpa kidogo Adamu naye ale.

Tunayajua matokeo vizuri sana: uhusuiano baina ya Mungu na mwanadamu uliovunjika, mahusiano baina ya wanadamu yaliyovunjika pia, ugumu katika kazi na uchungu wa uzazi, kufukuzwa katika bustani ya Eden, ongezeko la viwango vya kina cha dhambi na kuvunjika kwa ndani, na mwisho mauti ya mwili. Twaujua ulimwengu huu kwa maana tuliurithi kutoka kwa Adamu na hawa. Mpaka kufikia Mwanzo sura ya 6, wanadamu wameujaza ulimwengu na kitu kilicho tofauti kabisa na mfano wa Mungu – vurugu na ufisadi.

Angali amehuzunishwa na dhambi za wanadamu, Mungu aliamua kuisafisha dunia kwa gharika na kuianzisha upya. Aliwaacha hai Nuhu na familia yake, akiwapa amri ya msingi sawasawa na ile ya Adamu na Hawa: "Zaeni mkaongezeke na kuijaza dunia" (Mwanzo 9:1). Kwa mara nyingine tena, Mungu anaonyesha shauku yake ya kuwabariki wanadamu na kuwaamuru kuijaza dunia na sura yake.

Lakini kama ilivyokuwa kwa Adamu na Hawa, uzao wa Nuhu nao walishindwa. Kwanza, mwana wa Nuhu, Hamu alifanya dambi ya uzinzi, na baadae, badala ya kusambaa na kuujaza ulimwengu, Familia ya Nuhu ikaishia Babeli. Ili kujitengenezea jina, wakaanza kujenga mnara kuelekea mbinguni. Mungu akaingilia kati, akachanganya lugha yao, na ubinadamu ukagawanyika katika lugha nyingi tofauti na makundi tofauti.

Kilichofuata, Mungu akawachagua Israeli kama watu wake maalumu wa kufuata njia zake na kuleta Baraka kwa ulimwengu. Wana wa Israeli walipokwenda Misri kujikinga na njaa kali, "walizaliana na kuongezeka sana, wakawa wengi na wenye nguvu mno, wakaenea kila mahali nchini Misri" (Kutoka 1:7). Na

sasa yale maneno yafahamikayo ya uumbaji yaliielezea Israeli: "Zaeni mkaongezeka na kuujaza ulimwengu." Kazi haikubadilika – waisraeli wanapaswa kuijaza nchi yao na watu wenye kufana na Mungu. Nini kilichofuata baadae?

Historia ya Israeli katika Agano la Kale huleta usomaji wa huzuni. Badala ya kuijaza nchi na mfano wa Mungu, waisraeli walijilimbikizia utajiri wa mali na kuwekeza katika sifa za kijeshi (Isaya 2:7). Mbaya zaidi, waliabudu miungu, wakajihusisha na vurugu pamoja na uzinzi. Kama vile Mungu alivyowafukuza Adamu na Hawa kutoka katika bustani ya Edeni, Mungu aliwafukuza wana wa Israeli kutoka katika nchi yao ya ahadi. Kila kizazi kilifanya hivyo hivyo, kushindwa kuujaza uumbaji wa Mungu na mfano wake – mpaka pale alipokuja Yesu kama Adamu wa pili.

**Yesu: Mfano Kamili wa Mungu**

Tofauti na mwanadamu mwingine, Yesu alimfanana Mungu! Kama Yohana asemavyo, "Hakuna mtu aliyemwona Mungu kamwe. Mwana wa pekee aliye sawa na Mungu ambaye ameungana na Baba, ndiye aliyetujulisha habari za Mungu" (1:18). Kwa

maneno mengine, ni wale waliomuona Yesu walimuona Mungu. Na sivyo hivyo tu, walipata kuona muonekano kamili wa kipi Mungu alitazamia kwa kila mwanadamu aliye hai.

Mtume Paulo alimlinganisha Yesu na Adamu, akielezea kwamba Adamu wa kwanza alipoleta dhambi duniani, mauti ilisambaa kwa uanadamu wote. Tofauti ni kwamba, Adamu wa pili, Yesu Kristo, alileta msamaha wa dhambi na uzima wa milele. Yesu hutukomboa kutoka katika nguvu ya dhambi kila siku ili kwamba "tutawale katika maisha," tukiwa na mfano wa Mungu badala ya wa Adamu (Warumi 5:17). Roho Mtakatifu aishiye ndani yetu hufanya maisha haya ya ushindi yawezekane.

Yesu hakuja tu kufa kwa ajili ya dhambi zetu; alikuja kurejesha uumbaji wote chini ya utawala wa Mungu. Paulo anamuunganisha Adamu na Yesu anaponukuu Zaburi 8:6: "Ulimpa madaraka juu ya kazi zako zote; uliviweka viumbe vyote chini ya mamlaka yake." Kila alichoshindwa kufanya Adamu wa kwanza – kutawala vizuri uumbaji wote na kuijaza dunia na mfano wa Mungu – Yesu, Adamu wa pili, atafanikiwa kutimiza. Kila ali-chotambulisha Adamu wa kwanza katika dunia

yetu – dhambi, mateso na mauti – Adamu wa pili atakishinda.

Baada ya Yesu kumshinda kila adui, akiwemo mauti, atafanya uumbaji mpya kwaajili ya watu wake kuishi. Uwepo wa Mungu mwenyewe miongoni mwa watu wake ndiyo kitakuwa kilicho bora kuliko katika huu uumbaji mpya. Atafuta kila chozi katika kila jicho. Kifo kitakuwa jambo la kale. Hapana kuomboleza. Hapana kulia. Hapatakuwa na maumivu tena. Hakuna kisicho kisafi kitakachoingia ndani ya uumbaji mpya. Hayupo atakayetenda dhambi tena (Ufunuo 21:22). Utume umekamilika!

**Uanafunzi: Kuwa Kama Yesu**

Ujumbe wa Biblia kwa ujumla uko wazi: Yesu Kristo atautengeneza ulimwengu wetu uliovunjika na kuujaza na sura ya Mungu. Tangu siku alipoumba wanadamu, Mungu alitafuta kuumba watu wenye kuwaza, kutenda na kupenda kama yeye. Kama Paulo asemavyo, "Maana hao aliowachagua tangu mwanzo, ndio aliowateua wapate kufanana na Mwanae, ili Mwana awe wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi" (Warumi 8:29). Uanafunzi, hali hii ya sisi kusogezwa karibu

na Kristo mpaka kuwaza, kutenda na kupenda kama yeye, ni mpango wa Mungu kwa maisha yako katika hali yake ya kimsingi Zaidi! Lakini sasa, twaanzaje safari hii ya kumfuata Kristo? Ni kipi tutakutana nacho njiani? Na tunawasaidiaje wengine wamfuate Kristo pamoja nasi? Soma upate kugundua nini Baba ameweka ghalani kwaajili yako katika safari hii ya kushangaza.

# Sura ya 1

## Mwanaume Huyu ni Nani? Kumtambulisha Yesu (Marko 1:1–8:21)

"Je, waweza kuwa mwanafunzi wangu?" aliuliza mwanafunzi mkubwa chuoni kwetu. Yeye na mkurugenzi wa huduma ya kampasi walinikabili kutoka katika kochi la chumba changu bwenini. Nikadhini alimaanisha mimi kujitolea katika kumuona kila wiki kwa ajili ya mafunzo. Kwa pamoja tungefanyia kazi mrorongo wa vijitabu vya mafundisho ya Biblia. Tungesali pamoja, kuhudumu pamoja na kushiriki injili mara kwa mara. Japo nilikataa ombi hili, safari yangu binafsi ya uanafunzi ndio ilianzia hapa.

Je, uanafunzi unapaswa ufananeje? Mara nyingi marekani, tunarukia katika machapisho ya mtu mwingine ya nyenzo na mbinu za ufundishaji kabla hata hatujaainisha ama kutambua lengo. Kama sura iliyopita ilivyoelezea wanafunzi wanatafuta kujifunza njia za Yesu na kuwa kama yeye. Mtume Paulo asingeweza kuiweka kiurahisi kuliko

hivi: “Niigeni mimi kama nami ninavyomwiga Kristo” (1 Wakorintho 11:1)

Kwa kuwa Yesu alirejea katika mkono wa kuume wa Baba, twaweza kuchagua kumfuata mtu anayeonekana kufanya kazi nzuri ya kumfuata. Wakati huo huo, tunatakiwa tufungue zile injili nne (Mathayo, Marko, Luka and Yohana) ili mara kwa mara tumtazame Yesu. Tunapaswa kujishughulisha zaidi kwa maswali kama “Yesu aliishije?” na “Yesu alikwenda wapi?” na “Aliwafundisha nini wafuasi wake?” Picha ya Yesu katika injili hutuelekeza katika uelekeo sahihi.

Marko hututambulisha kwa wanafunzi Kumi na mbili wa kwanza wa Yesu, ikielezea simulizi zao ili kuonyesha jinsi wanafunzi wanavyojifunza kumfuata Yesu katika hatua tatu zifuatavyo:

1. Kwanza, mwanafunzi ni lazima atambue *Yesu ni nani*.
2. Kisha Yesu anawatia changamoto wanafunzi *kuuelewa na kuukubali utume wake*.
3. Mwisho, ni lazima mwanafunzi *abaki kuwa mwaminifu* kwa maana utume huo hupelekea *katika mateso* yasiyozuilika.[1]

Katika Marko, kila mmoja ameshindwa kuelewa nini Yesu anaongelea kuhusu huduma ya Masihi. Mwishoni, ni Yesu tu abakiaye mwaminifu!

Je, tunaamini ya kuwa twaweza kumfuata Yesu vyema kuliko wanafunzi Kumi na mbili? Marko anatuacha tulitafakari swali hili. Kama vile wao, nasi tunapata shida kukubali Yesu kweli ni nani. Kama vile wao, tunapata shida kukubali asili ya huduma yake. Na kama vile wao, tunapata shida kubakia waaminifu. Kwa maana hakuna mwingine isipokuwa Yesu aliyeyapatia yote hayo, kiuwazi kabisa sasa tunaona namna gani tunahitaji kumtegemea yeye.

**Masihi Aliyetiwa Nguvu na Roho (1:1-15)**

Kabla ya wanafunzi kumfuata Yesu, walitakiwa *kumtambua Yesu ni nani*. Msitari wa kwanza kabisa wa Marko unamtamka Yesu kuwa ni Masihi na Mwana wa Mungu. Mamia ya miaka kabla, nabii Isaya alitamka kusema kuwa watu watajua Masihi kaja kwa maana watauona uwepo wa Roho mtakatifu ndani yake. Isaya akaandika, "Roho ya Mwenyezi-Mungu itakaa kwake, roho ya hekima na maarifa, roho ya shauri

jema na nguvu, roho ya ujuzi na ya kumcha Mwenyezi-Mungu" (11:2).

Katika kubatizwa kwa Yesu, anga lilipasuka na Roho akashuka juu yake katika muundo wa njiwa. Sauti ya Mungu ikaunguruma, ikimtangaza kuwa "Mwanaye mpendwa" ambaye "alipendezwa naye" (1:11). Baadaye, kuwathibitishia mji alioishi kuwa yeye ni Masihi, Yesu akamnukuu Isaya: "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwani ameniweka wakfu niwaletee maskini Habari Njema. Amenituma niwatangazie mateka uhuru wao, na vipofu watapata kuona tena; amenituma niwakomboe wanaoonewa" (Isaya 61:1; Luka 4:16-21).

Baada ya kumpokea Roho, Yesu alivumilia siku arobaini nyikani. Hapa shetani alimjaribu ili aachane utume wake wa kuukomboa ulimwengu. Kwa kubakia kwake katika kumtegemea Roho, Yesu aliyashinda majaribu na kuanza huduma muda mfupi baadaye.

**Masihi Astahiliye Kufuatwa (1:16-20)**

Yesu aliwatafutia wafuasi wake wa kwanza katika bahari ya Galilaya – ndugu wawili, wote wavuvi. Yesu alipomuita Petro na Andrea kuja kwake, akiwaahidi kuwafanya wavuvi wa watu, aliwaonyesha lengo la msingi la uanafunzi:

kuwakamata watu kwaajili ya Kristo. Simulizi hii hii katika Luka, Yesu pia alifanya kitu cha kushangaza (Luka 5:1-11).

"Petro, shusha nyavu zako mbele kidogo," Yesu alimuita. Petro alitii, japo alijua hamna kitakachopatikana. Sekunde chache baadae, akihisi kuvutwa kwa nyavu, kisha mvuto ukazidi kuongezeka. Petro na wenzake wakaanza kuvuta kwa kasi samaki wengi kiasi cha mitumbwi yao miwili kutaka kuzama! Somo zuri kiasi gani – walikamata samaki wengi kwa msaada wa Yesu wakiwa hawakupata samaki hata mmoja siku moja kabla. Wanadamu wa kawaida waovu, ambao wao peke yako mara nyingi hushindwa, wanafanikiwa pale Yesu anapojumuika nao. Mara moja tu ndugu hao wawili wakaziacha nyavu zao; kwa maneno mengine, waliacha kazi zao na vipato vyao na kumfuata Yesu.

Baadaye kidogo, Yesu akawaona ndugu wengine wawili. "Nifuateni," akawaita Yakobo na Yohana. Kama vile Petro na Andrea, hawa ndugu wawili nao waliona kitu maalumu ndani ya mwanaume huyu aitwaye Yesu. Siyo tu waliacha mitumbwi na nyavu zao na biashara yao iliyooneka kuchanua (kumbuka uwepo wa "mtumishi aliyeajiriwa"), wakamuacha pia

baba yao. Ni kama hali fulani ya kushtua, hata kuaibisha kidogo! Ni "kitu kipi hiki maalumu" waliona ndani ya Yesu?

**Masihi Mwenye Mamlaka na Nguvu (1:21-45)**

Watu walitambua vitu viwili maalumu kuhusu Yesu alipokuwa akifundisha hekaluni Kapernaumu. Kwanza, ufundishaji wa Yesu ulionekana tofauti na yale ambayo wamekuwa wakisikia kwa maana alifundisha kwa *mamlaka*. Marabi ama waalimu wengine walijikakamua ili kuhakikisha watu muhimu wanawakubali, lakini mafundisho yao yalishindwa kushawishi. Yalikuwa butu, yasiyo na uhai, yasiyo na umuhimu. Hakuna aliyewahi kumshutumu Yesu kwa kitu cha namna hiyo.

Pili, watu waliitambua *nguvu* ya Yesu. Yesu alipofundisha, roho za ulimwengu zilitetemeka! Mapepo yalimuogopa, kana kwamba yalimjua. Watu wengi waliyaogopa mapepo, aliyaamuru kwa ujasili na yakatii. Yesu pia aliitendea kazi nguvu yake katika magonjwa. Homa kali ilimkamata mama mkwe wa Petro. Yesu alimshika tu mkono kiurahisi na homa ikamwachia mara moja. Wagonjwa wa aina zote na wenye mapepo walikusanyika kwake, na akawaponya wote. Aliwaponya

hata wakoma, waliotengwa mbali na jamii wakiteseka katika hali zao mbaya sana.

Je, wanafunzi wenye uwezo kama Petro, Andrea, Yakobo na Yohana walitakiwa wahitimishe nini kuhusu Yesu? Angeweza kuwa Masihi. Angeweza kuwa Mwana wa Mungu! Bila shaka alionekena vyovyote vile alivyokuwa kwa kila aliyekutana naye.

**Masihi Mvunja Kanuni (2:1–3:6)**

Lakini si kila mmoja alimkubali Yesu kama Masihi mwana wa Mungu. Cha kushangaza, wakati wenye dhambi wakirundikana kwa Yesu kwa ajili ya msaada na uponyaji, migongano ilizuka kati ya Yesu na wanadini.

Yesu alipata kuwa na mgongano wake wa kwamza na wanadini alipokuwa akifundisha katika nyumba ya Petro kule Kapernaumu. Kundi kubwa la watu likakusanyika, wengi kiasi kwamba waliomleta mwenye kupooza walishindwa kuingia. Hakuna shida! Wakapanda juu ya nyumba na kutoboa tundu wamshushe kutoka juu. Yesu alipomponya mtu yule na kumsamehe dhambi zake, wanadini walijua anafanya mambo ambayo Mungu tu ndo awezaye kufanya. Lakini badala

ya kumsadiki kama Mwana wa Mungu, walimshutumu kwa udanganyifu.

Mara nyingine, Yesu akamuita mtoza ushuru aitwaye Lawi amfuate. Wayahudi wa nyakati hizo waliwachukulia watu kama Lawi watu wabaya kuliko wabaya. Wanadini walilalamika kuhusu Yesu kuwa na muda na "watoza ushuru na waovu" (2:16). Yesu akaelezea: "Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali wasiojiweza; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi. Sikuja kuwaita wenye haki, bali waovu!" (2:17).

Mara nyingi wanadini hukasirika pale watu "wanapovunja sheria." Walimzonga Yesu kwasababu wanafunzi wake hawakufunga kama wale wa Yohana na wa mafarisayo. Yesu akawajibu kuwa wanfunzi wake hawakuhitaji kufunga angali akiwa pamoja nao.

Kisha mafarisayo wakawakamata wanafunzi wa Yesu wakitembea katika shamba siku ya Sabato, wakiokota nafaka na kuzila. Hii haikuwa kinyume na sheria; ilikuwa ni "uvunaji"! Wanafunzi, hali kadhalika, hawakuvunja roho ya sheria ya Sabato. Walivunja tu jinsi ambavyo mafarisayo wamekuwa wakiifanya. Yesu anadai kuwa

yeye ni “Bwana wa Sabato,” huru na kanuni zilizotengenezwa na mwanadamu (2:28).

Katika Sabato nyingine, Yesu akakutana na mwanaume mwenye mkono mbovu katika hekalu. Macho yote yakawa kwa Yesu. Je, atavunja tena sheria kwa kuponya katika siku ya Sabato? Yesu alijisikia kusononeka sana kwa jinsi watu hawa walivyothamini sana sheria zao kuliko mahitaji ya watu. Kwa kumuamuru mtu yule anyooshe mkono wake, Yesu akawa amemponya kabisa. Kwanzia wakati huo mafarisayo walianza kupanga njama za kumuua Yesu.

Vyovyote Yesu alivyokuwa, hakika hakuonekana kama kiongozi wa kidini wa Israel! Alifundisha kwa mamlaka. Aliyaamuru mapepo na yakatii. Aliitendea kazi nguvu ya uponyaji. *Alithamini watu kuliko kanuni* na tamaduni za wanadamu. Makundi mawili yakaanza kuundwa – baadhi walipenda walichokiona na kumfuata Yesu, na wengina wakamchukia Yesu na kuanzisha njama za kumharibu.

**Masihi Mtenda Miujiza (3:7–6:6)**

Watu walipokuwa wakichagua pande, Yesu akachagua wanaume kumi na mbili kati ya kundi la watu wawe wafuasi wake wa karibu. Alitaka kundi hili maalumu “kuwa naye,”

maana kiurahisi kabisa kuwa na Yesu ni sehemu ya uanafunzi (3:14). Aliwapa utume wake wa kuihubiri injili ili kwamba wangeendeleza huduma yake pindi ambapo hatakuwa akitembea miongoni mwao tena. Pia aliwapa mamlaka yake ya kutenda miujiza ya kushangaza kama aliyofanya mwenyewe. Mfano, alitoa mapepo kuthibitisha uwepo wa Mungu na watu.

Muda kidogo, Yesu aliwajaribu wanafunzi kumi na mbili ili kuona kama kweli wameelewa yeye ni nani. Baada ya siku ndefu ya mafundisho, Yesu aliwapeleka nje kidogo baharini mbali na kundi la watu, ambapo haraka sana akalala usingizi ndani ya mashua. Upepo ukazuka. Mawimbi yakainuka na kushuka, yakigonga pande zote za mashua. Mashua ikaanza kujaa maji. "Mwalimu, haikupi shida kuona tunaangamia?" wakalia (4:38). Yesu alihitaji tu kusema maneno mawili tu – "Nyamaza, utulie!" – ili dhoruba iishe kabisa. Baada ya kuikemea bahari, Yesu akawakemea wanafunzi kumi na mbili. "Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?" (4:40). Baada ya kushuhudia mengi ya Yesu, bado hawakuamini kikamilifu ya kuwa yeye ni Mungu. Ingawa walikuwa wakifanya

maendeleo vizuri katika hilo. Swali lao lililoshangaza lilithibitisha kuwa walijua Yesu siyo mwanadamu wa kawaida: "Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?" (4:41).

Yesu aliwajibu swali lao kwa kuwaonyesha nguvu zake hata kwa yale yasiyowezekana. Walipofika ng'ambo nyingine ya bahari, mwanaume kichaa aliyetawaliwa na mapepo alimkabili Yesu. Akiwa uchi, mwenye macho yenye ukichaa na vipande vya minyororo iliyakatikakatika mikononi, alipiga magoti mbele za Yesu. Moja kwa moja mapepo ndani yake yakamtambua Yesu, yakimuita, "Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu!" (5:7). Yesu akayatuma mapepo katika kundi la nguruwe, lililopagawa na mapepo na kuteremka chini hadi baharini na kufa.

Akiwa anaelekea kwa Yairo, ambaye bintiye alikuwa anakabiliwa na mautii, Yesu alikutana na mwanamke aliyeteseka kwa kutokwa damu miaka kumi na mbili. Alitumia pesa zake zote kwa madaktari lakini badala ya kupata afadhali, hali ndiyo ilizidi kuwa mbaya. Mwanamke yule aliamini ya kuwa akishika tu pindo la vazi la Yesu, angeweza kupona. Yesu akiwa ameshangazwa na imani yake, alimponya kabisa.

Lakini alipokuwa akiongea na mwanamke yule, wajumbe walifika na kumwambia Yairo kuwa binti yake amekwishakufa. Kuponya wagonjwa ni jambo moja. Lakini kufufua wafu? Ndiyo kama haiwezekani zaidi! "Usiogope, amini tu," Yesu akamtia moyo Yairo (5:36). Kwa imani, Yairo akamfuata Yesu nyumbani kwake. Kama ilivyokuwa katika bahari kali, Yesu alitamka maneno mawili: "Binti, amka," na, kweli akaamka (5:41). Wanafunzi walipomuona Yesu akituliza bahari, akiamuru mapepo, akiponya wagonjwa na hata kufufa wafu, walimshuhudia *akifanya miujiza* ambayo Mungu tu ndiye awezaye fanya.

**Masihi Abadilishaye Mioyo (6:7–8:21)**

Baada ya wanafunzi kukaa na Yesu muda mrefu, aliwaagiza waende kuhubiri injili peke yao, kutoa mapepo, na kuponya wagonjwa. Yesu alimtegemea Mungu na watu wake kukutana na mahitaji yake, na aliwaambia wanafunzi wake wafanye hivyohivyo. "Msichukue chochote bali fimbo ya kutembelea – wala chakula, wala fedha, wala kubadilisha mavazi! Bakini katika nyumba ya kwanza mtakayokuwa mmeingia," Yesu aliwaelekeza.

Japo walikuwa hawajapata kumtambua Yesu ni nani kikamilifu, walifuata njia aliyowatangulia.

Kama vile Yesu, wanafunzi walifukuza mapepo na kuponya wagonjwa. Lakini hata walipokuwa wakitenda miujiza hiyo, wanafunzi waliendelea kupata shida kuamini kikamilifu ya kuwa Yesu ni Mungu. Walimuona akiwajali makundi waliokuwa wakimfuata kama mchungaji. Alizishibisha njaa zao za kiroho kwa mafundisho yake na njaa zao za kimwili kwa mkate pale nyikani. Alilisha watu wapatao 5,000 kwa mikate mitano tu na samaki wawili. Wanafunzi walipoanza kukusanya ndoo kumi na mbili za masalia ya chakula, hakika walianza kuelewa ya kuwa ni Mungu tu mwenye kuweza kufanya muujiza wa namna hiyo.

Lakini hata baada ya haya yote, bado wanafunzi waliendelea kukataa kumwamini Yesu kikamilifu. Akiwa amechoka baada ya siku ndefu na makusanyiko ya watu, Yesu aliwaambia wale Kumi na mbili watangulie na safari baharini huku yeye akijitenga kidogo ili asali. Baadaye, Yesu alipotembea juu ya maji ili kuwafikia na kuungana nao safarini, wanafunzi wake walilia kwa hofu, “Ni mzimu!”

Akituliza hofu zao, Yesu akapanda kujumuika nao mashuani.

Kwa mara nyingine walimshuhudia Yesu akitawala juu ya asili/uumbaji. Ni Mungu pekee aitawalaye asili. Lakini badala ya kuamini katika Yesu, "wakashangazwa sana, kwa kuwa hawakuelewa nini hasa kilitokea kabla kwa habari ya mikate, lakini mioyo yao badoo ilifanyika migumu" (6:51b-52). Uanafunzi – kujifunza kumfuata Yesu – hutokea katika mwendo mdogo unaokera. Hata pamoja na hawa ndugu kuendelea kuona na kuelewa zaidi kuhusu Yesu, bado walikuwa na umbali mrefu wa kwenda!

Muda kidogo, wanafunzi wakapata mtihani mwingine baharini. Mbele ya safari wakagundua kuwa walikuwa wamesahau kuja na mikate safarini. Wangemuamini Yesu kuwapatia mikate kama alivyofanya kwa wale 5,000 nyikani. Badala yake, walihofu na kupigana wao kwa wao. Yesu akawaambia wanatakiwa wahofie zaidi mambo ya kiroho kuliko kuhofia mikate ya kula. Lakini wanafunzi hawakumuelewa, wakidhani amesononeshwa na wao kusahau kuleta chakula. Badala yake, Yesu akawakemea kwa

kutokuamini kwao: “ndugu zangu msihofie chakula. Nilidhani hilo tulishalishughulikia!”

Tunajiuliza, “Ni kwa namna gani katika ulimwengu huu mioyo ya hawa wanafunzi ilijawa ukorofi?” Lakini kisha tunajitazama sisi pia na kujiuliza, “Je, imani yetu ni kubwa kuliko yao?” Yesu aliwapa wale kumi na mbili ushahidi wote ili waweze kuwa hitimisho sahihi. Yesu aliwakemea kwa kuwa kama kizazi chao chote – kuwa viziwi na vipofu wa kazi ya Mungu. Kupata “masikio ya kusikia na macho ya kuona” ingeweza kuchukua muda kama ilivyo kwetu (8:18).

## Maswali kutoka Sura ya 1

1. Soma Marko 1:1—8:21. Tunza kumbukumbu ya chochote kin-achoonekana kuwa cha muhimu. Je, una maswali gani?

2. Kipi kwa Yesu kinakuvutia zaidi? Kipi kinakusumbua?

3. Yapi uliyochunguza kwa wanafunzi yakupayo shida? Je, watambua tabia yoyote miongoni mwa hizi ambazo zimo maishani mwako?

4. Yesu alijitolea katika kutimiza kusudi la Baba, siyo kuwapendeza watu waliomzunguka. Alikuwa tayari kwenda kinyume na maoni yaliyojulikana ulimwenguni ili tu kumpendeza Baba yake. Vipi kuhusu wewe? Kuna ugumu gani umekutana nao ama unaweza kukutana nao kutoka kwa watu wengine ukimfuata Yesu?

5. Kwa maneno yako, muelezee Yesu kutokana na injili ya Marko.

# Sura ya 2

## Anafanya nini? Umisheni wa Yesu (Marko 8:22–10:52)

Yesu ni nani? Ni lazima tujibu hili swali kabla hatujaweza kumfuata Yesu popote. Yeye ni mwana wa Mungu. Yeye ni Masihi aliyekuja kuwaokoa watu mbali na dhambi zao, awezaye kutenda miujiza ambayo Mungu pekee ndiye mwenye kuifanya. Cha muhimu zaidi, anafanya muujiza wa kubadilisha mioyo ya watu wamuamini.

Lakini kama Yesu alikuwa Masihi, hakuyafikia matarajio ya watu hata kidogo. Njia yake ilikwenda tofauti kabisa na njia ya watu wa kidini. Na matokeo yake walimpinga. Tutarajie nini ikiwa Yesu ataendelea na njia hii? Twaweza tu kutarajia migongano mikubwa zaidi!

Yesu hakuwakwaza tu wanadini, bali wale Kumi na mbili pia, waliosumbuka kuielewa kazi yake duniani. Mara tatu Yesu aliwaambia kuhusu ujio wa kukataliwa kwake, kifo na ufufuo wake. Mara tatu! Kushindwa kwa wanafunzi wake kuitikia katika imani

kwathibitisha hawakuelewa nini kusudi lake la kuja duniani. Ni kama vile tunaweza kusikia mawazo yao yakilia namna hii, "Hivi tumejihusisha na nini katika ulimwengu huu?"

**Kuanza Kuuona Umisheni (Marko 8:22-30)**
Mara wanafunzi walipoanza kumuona Yesu ni nani, walihitaji kujibu swali jingine: "Kazi ya huyu Masihi ni nini?" mtazamo wao wa Yesu ulikuja kupata mkazo taratibu sana, kama yule mtu kipofu ambaye Yesu alimponya kwa hatua. Kiajabu, Yesu alitemea macho ya kipofu na kumuwekea mikono. Badala ya huyu mtu kupokea kuona, alibakia kuona kama ukungu. Watu kwake walionekana kama miti inayotembea. Kisha Yesu akamuwekea mikono tena, na wakati huu sasa mwanaume huyu alipata kuona kikamilifu.

Wakielekea mji mwingine baada ya uponyaji, Yesu akawauliza wanafunzi wake, "Nyinyi mwasema mimi ni nani?" Pasipo kusita, Petro akajibu, "Wewe ndiye Masihi" (8:29). Kama vile yule kipofu, wanafunzi waliona baadhi ya kweli kuhusu Yesu, lakini uelewa wao ukabaki hafifu. Uanafunzi huchukua muda. Hatufanyiki kama Yesu mara moja tu. Badala

yake, tunakuwa taratibu katika uelewa wetu wa Yesu ni nani na jinsi gani ya kuishi kama yeye.

**Umisheni: Kuteseka Sasa, Utukufu Baadaye (Marko 8:31–9:29)**

Petro anaonyesha ni kwa kiasi gani wanafunzi walipaswa kueendelea kujifunza. Mara baada ya ukiri wake wa imani katika Yesu, aliangukia katika mashaka. Yesu alianza kuwafundisha wanafunzi wake ya kuwa angepitia mateso mengi, angepata kukataliwa na viongozi wa dini, kufa, na baada ya siku tatu kufufuka kutoka kaburini. Kama vile watu wa kidini wa wakati huo, wanafunzi walitazamia mfalme mwenye kushinda. Walitazamia mtu ambaye angewafukuza warumi waliochukiwa kutoka katika nchi yao. Walitaka utawala wa Masihi uwaletee amani ya milele na mafanikio. Hakuna aliyetazamia Masihi mwenye kukataliwa na kuteswa. Yesu alisema Masihi hatateswa tu, bali atauawa!

Petro mjuaji akamkemea Yesu, "Hapana, Yesu! Hutateseka wala kufa!" Yesu akajua kuwa Shetani alikuwa akimjaribu kupitia Petro ili ayaepuke mateso na kufanyika kuwa yule mfalme ambaye kila mmoja alimtumainia. Akamkemea Petro, "Rudi nyuma yangu,

Shetani, haufikirii yaliyo ya Mungu bali yale yalio ya wanadamu!"

Ni lazima njia ya wanafunzi ifanane na ya Bwana wao. Yesu aliwaambia makutano na wanafunzi wake:

> Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake na anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili, huyu ataisalimisha. Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake? Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu. (8:34-38)

Yesu anatoa machaguo mawili kwa wale watakao kumfuata. Wanaweza kujikana wenyewe na kupata hasara sasa ili kupokea

utukufu baadaye. Kwa upande mwingine, wanaweza kujitahidi kuupata utukufu hapa duniani, ili kuishia katika aibu na hasara katika umilele.

Wakati machaguo hayo yakionekena kuwa na utulivu fulani, Yesu aliwapa wanafunzi wake kionjo cha tumaini la utukufu ujao. Akiwachukua Petro, Yakobo na Yohana kwenda mlimani, ghafla Yesu akaanza kung'aa kwa "Nuru ing'aayo" (9:3). Musa na Eliya wakajumuika naye. Wingu likawazunguka na sauti ikiunguruma, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikilizeni" (9:7). Petro hakuwahi kusahau hilo jambo, na hata kuandika kuhusiana nayo miaka kadhaa baadaye katika 2 Petro. Kuuona utukufu ujao kulimpa ujasiri wa kukabiliana na majaribu ya maisha yake ya hapa duniani.

### Umisheni: Kutumika kwa Unyenyekevu (9:30–10:31)

Yesu akawaondoa wanafunzi wake kutoka katika kusanyiko ili kuwaonyesha tena jinsi gani itakavyompasa kuteseka, kufa na kufufuka tena. Kwa mara ya pili, wanafunzi walishindwa kuelewa. Waliogopa sana kumuuliza Yesu alikuwa anamaanisha nini. Badala yake,

walipokuwa wakisafiri njia iendayo katika msalaba wa Yesu, walibishana kwa habari ya mwanafunzi yupi kati yao alikuwa bora zaidi!

Waweza kumsikia Yesu akishusha pumzi nzito? Aliwaonya, "Yeyote atakaye kuwa wa kwanza ni lazima awe wa mwisho na awe mtumwa wa wote." Kisha akaweka mtoto mbele yao. Ikiwa kweli wanafunzi walitaka kufanyika wakubwa, wasiwatumikie matajiri, wenye nguvu, akili na walio wazuri. Badala yake, wawajali wanyonge, wanyenyekevu, wasioonekana kuwa na maana na watoto wadogo.

Yesu hakuzungumza sana kabla wanafunzi hawajaonyesha tena ni kwa kiasi gani hawakumuelewa. Wazazi waliwaleta watoto wao kwa Yesu ili awabariki, lakini wanafunzi walijaribu kuwaondoa. Wakati huu sasa, Yesu mwenye uvumilivu akapatwa na hasira. "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa Mungu ni wa watu kama hawa," alisema (10:14). Pamoja na yote Yesu aliwafundisha, wanafunzi waliendelea kuwa kama viongozi wa kidini wenye majivuno badala ya kuwa kama Yesu. Ni wanafunzi walio na kasi ya kujifunza ndogo kiasi gani hawa!

Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakishuka barabarani tena, kijana mdogo tajiri akawafuata. Alitaka kweli kumfuata Yesu – mpaka alipojulishwa gharama yake. "Nenda, uza mali zako zote na uwape masikini, na utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate," Yesu alimtia moyo (10:21). Kijana aliondoka kwa huzuni, akiwaza, "Ningekufuata Yesu, kama isingemaanisha kubadilisha maisha yangu kiasi hicho chote. Lakini kutoa kila kitu? Hiyo ni gharama ya juu sana!"

Kwa mara ya kwanza, Petro akafanya uchunguzi wenye maana: "Tumeacha kila kitu kukufuata!" (10:28). Na Yesu akaahidi:

> Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele. (10:29-30)

Tunashangazwa na uelewa wa chini wa wanafunzi, lakini angalau walipatia kwa usahihi eneo gumu kuliko. Pasipo kusita, waliacha kila kilicho chema kwao ili kumfuata Yesu.

**Umisheni: Kutumika kwa Kuacha Kila Kitu (10:32-45)**

Kwa mara ya tatu na mwisho, Yesu alitabiri njia yake ingempeleka wapi: "Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalemu; na Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi, nao watamhukumu afe, watamtia mikononi mwa mataifa" (10:33-34). Na kwa mara ya tatu, wanafunzi wake walimuitikia kwa mtazamo wa kibinadamu badala ya wa kimungu.

Yakobo na Yohana wakamuendea Yesu na ombi. "Yesu, tukifika Yerusalemu na watu wakakuvisha taji la ufalme, twaweza kujaza nafasi za uweza wa juu sana katika ufalme wako?"

Kwa mara nyingine na kwa uvumilivu, Yesu akawasahihisha:

> Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa

> nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote. Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi. (42-45)

Hapa tunakutana na fundisho lingine muhimu kuhusu uanafunzi. Yesu si kama wale wafalme wengine wa ulimwenguni. Ufalme wake pia hautendi kazi kama falme zingine za ulimwengu huu. Njia yake ya kuishi inasimama juu – tofauti – na kila njia nyingine ya maisha. Wale wamfuatao ni lazima wakubali mabadiliko.

**Kuuona Umisheni Wazi Zaidi (10:46-52)**

Kabla ya Yesu kutabiri kifo chake kwa mara ya kwanza, alimponya mwanaume kipofu katika hatua tofauti. Sasa baada ya kutabiri kifo chake kwa mara ya tatu, aliponya mwanaume mwingine kipofu. Safari hii uponyaji wote ulifanyika mara moja. Vipofu wote wawili hutuonyesha vile uanafunzi unafanyikaje. Wafuasi wa Yesu walianza kuona, na siku moja

wangepata kuweza kuona kiroho kikamilifu. Baada ya kupata kuona, mwanaume kipofu alimfuata Yesu “katika njia” kama ambavyo angetakiwa mwanafunzi yeyote mwema (10:52). Na kadri wale Kumi na mbili walivyozidi kuona wazi, wangelimfuata Yesu kwa karibu zaidi na katika njia yake hiyohiyo.

## Maswali kutoka Sura ya 2

1. Soma Marko 8:22 hadi 10:52. Weka kumbukumbu ya kila uchunguzi uonekanao kuwa wa muhimu. Una maswali gani?

2. Fikiria vile uongozi utendekavyo katika utamaduni wako. Elezea jinsi vile kiongozi awavyo katika sehemu ya ulimwengu wako.

3. Fikiria kuhusu Yesu alipojitabiria mara tatu kukataliwa kwake, kifo chake na kufufuka kwake. Miitikio ya wanafunzi huonyesha vile tusivyowaza kiusahihi. Na kila wakati, Yesu aliwafundisha kuhusu asili ya uanafunzi wa kweli.

- Katika 8:31-38 Petro alipinga kuteswa, kufa na kufufuka kwa Yesu. Kwa muitikio, Yesu alitufundisha kuyatoa maisha yetu na kumfuata. Tutapata mateso sasa lakini utukufu baadaye.

- Katika 9:27-31 wanafunzi walibishana kwa habari ya ni nani kati yao aliyekuwa mkuu. Kwa mitiko, Yesu alitufundisha kuwa twapata ukuu wa kweli kwa kuwatumikia wengine kwa unyenyekevu, hata wadogo na wale wasio na umuhimu.

- Katika 10:32-45 Yakobo na Yohana walitafuta nafasi za madaraka. Kwa muitikio, Yesu tena alitufundisha kutoa vyote tulivyonavyo na kisha kuwatumikia wengine.

Ni fundisho/mafundisho yapi kati ya haya unayohangaika nayo zaidi? Kwanini?

4. Wanafunzi walipoanza kumfuata yesu, hawakujua kuwa mwishoni wote wangekufa kwaajili yake. Wasomi wa Biblia huamini ni Yohana tu aliyekufa kifo cha kawaida. Sasa fikiria nyuma juu ya hali yako. Kumfuata na kumtumikia Yesu kumekusababishia mateso gani binafsi?

# Sura ya 3

## Wanafunzi Hubakia Waaminifu kupitia Mateso (Marko 11:1–16:8)

Je, wanafunzi kumi na mbili wangebakia waaminifu ikiwa njia ya Yesu ilielekea kupitia mateso? Walitambua Yesu ni nani – Masihi, Mwana wa Mungu. Lakini walimtarajia Masihi ambaye utume wake duniani ungehusisha kutawala mataifa yao na kuleta amani ya milele. Badala yake, waligundua kuwa utume wake ulihusisha kukataliwa, kuteseka na kufa. Utume wa Yesu ulipozidi kupata misukosuko sana, wanafunzi walitwanyika, wakimuacha Yesu apambane na kifo peke yake.

**Njia ya Mateso (11:1–13:37)**
Akiwafundisha wanafunzi na kuwaponya wagonjwa, Yesu alitembea kwa ukakamavu kuelekea Yerusalemu, mahali ambapo angefia. Kabla ya kuingia mjini, aliomba kuazimwa mwanapunda ili aingie naye katika malango ya mji. Makutano wakapaza sauti zao wakisema, “Hosana; ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina

la Bwana; umebarikiwa na ufalme ujao, wa baba yetu Daudi. Hosana juu mbinguni!" Yesu aliingia Yerusalemu kama aina ya Masihi aliyetarajiwa na wanafunzi. Alitokea kama mfalme mwenye kuabudiwa na wale waliompokea.

Lakini Yesu aliendelea kukatisha tamaa matarajio yao. Alipokula chakula cha pasaka na wale Kumi na mbili, aliwashtua kwa kusema, "Amin, nawaambia, Mmoja wenu, naye anakula pamoja nami, atanisaliti" (14:18). Wakaanza kuhuzunika, wakamwambia mmoja mmoja, "Je! Ni mimi?" Kila mmoja alitazama, kwa mfadhaiko, Yuda akichukua kipande cha mkate Yesu alichomchovyea. Katika siku za Yesu, marafiki wa karibu walichovya mikate katika bakuli la pamoja. Yuda aligeuza hii sherehe ya upendo kuwa tendo la usaliti.

Baada ya chakula walitembea katika Bustani ya Gethsemane, na Yesu akawashtua tena, akisema, "Mtaniacha ninyi nyote." Petro akambishia, "Katu! Hata kama kila mmoja akikuacha, sitakuacha! Hata kama itanilazimu kufa, nitakaa nawe." Baadaye kidogo, Yesu alipowaomba Petro, Yakobo na Yohana kukesha naye wakiomba, wakasinzia. "Simoni," akamwambia Petro, "Je! Simoni, umelala?

Hukuweza kukesha saa moja?" (14:37) Mara tatu wanafunzi walilala usingingizi wakati Yesu akiomba. Baadaye usiku huo Petro alimkana Yesu mara tatu hali akimjua yeye ni nani. Baada ya muda wote huu na Yesu, Petro alijikwaa tena kwa hatua ya kwanza kabisa ya uanafunzi – kukubali Yesu ni nani.

**Machaguo Mawili: Kujiokoa Mwenyewe au Kujikana Mwenyewe (13:37-16:8)**

Yuda aonyesha aina ya mwanafunzi anayegeuka moja kwa moja na kutomfuata Yesu. Mbaya zaidi, anageuka kuwa adui. Petro aonyesha aina nyingine ya mwanafunzi – yule ashindwaye lakini anapata msamaha. Mwishoni akarudi katika kumfuata Yesu. Safari hii aliutambua udhaifuu wake na kwa kiasi gani alihitaji msaada wa Mungu.

Kundi lilipowasili kumkamata yesu katika bustani ya Gethsemane, wanafunzi wote walikimbia isipokuwa tu Petro. Aliendelea kumfuata Yesu lakini akiwa katika umbali fulani. Walipofika katika nyumba ya kuhani mkuu ambapo kesi ya Yesu alianza, Petro alikaa uani. Akaja mmoja wa vijakazi wa Kuhani Mkuu, akamwona Petro akikota moto; akamkazia macho, akasema, Wewe

nawe ulikuwapo pamoja na yule Mnazareti Yesu" (14:67, mkazo ukaongezwa). Kumbuka Yesu kwanza alipowachagua wale Kumi na mbili kuwa wanfunzi wake, aliwachagua ili "wawe naye." Sasa kwa haraka Petro alikataa mahusiano: "Sijui wala sisikii unayoyasema wewe!" Petro akasogea pembeni kidogo karibu na malango ya ua. Mjakazi king'ang'anizi akamfuata, akitangazia watu, "Huyu ndugu ni mmoja kati yao" (14:69). Mara tena, Petro akakanusha maneno yake. Waliokuwa pembeni nao wakaungana naye kijakazi kumwambia Petro, "Hakika u mmoja wao, kwa sababu u Mgalilaya wewe" (14:70). Akimkana Yesu kwa mara ya tatu, Petro akaanza kulaani na kuapiza, "Simjui mtu huyu mnayemnena" (13:71).

Petro aliukana ukweli ili kuokoa maisha yake. Wakati huo Yesu alijikana, akaubeba msalaba wake, na kuyatoa maisha yake ili kutimiza kazi ya Mungu dunianai kwaajili yake. Wanafunzi waliendelea kutoonekana wakati wote wa simulizi ya kusulubiwa kwa Yesu. Wanapaswa kuwa wapi? Bila shaka wanapaswa kumfuata Yesu! Sasa kwasababu wale Kumi na mbili walipotelea, "wanafunzi" wengine walijaza nafasi zao, wakionyesha

jinsi ya kumfuata Yesu katika mateso. Yesu alipojikwaa kutokana na uzito wa msalaba, mwanaume aitwaye Simoni Mkerene alimsaidia mpaka eneo la masulubisho. Mapema kidogo, Yakobo na Yohana waliomba kuketi mahali pa mamlaka na heshima katika mkono wa kuume na wa kushoto wa Yesu. Katika mauti ya Yesu, kukawa na wahalifu wawili waliosulubishwa pamoja naye kulia na kushoto. Hapa ndipo walipopaswa kuwa – wakibeba misalaba yao wenyewe na kumfuata, siyo kutafuta nafasi za mamlaka na umaarufu.

Kundi dogo la wanawake lilimfuata Yesu mpaka msalabani, likisimama chini yake mpaka Yesu alipokufa. Mara nyingi wanawake huonyesha mfano chanya wa uanafunzi katika injili ya Marko. Hivyo tunatumaini kuwa, tofauti na wale Kumi na mbili, wao watabaki kuwa waaminifu. Baada ya Yesu kufa na kuzikwa, wanawake walielekea kaburini kuupaka marashi mwili wake. Badala ya kuukuta mwili wake, walimkuta malaika amekaa ndani ya kaburi tupu. "Naye akawaambia, Msistaajabu; mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyesulubiwa; amefufuka; hayupo hapa; patazameni mahali walipomweka" (16:6). Lakini malaika alipowaamuru kuwaeleza

wale Kumi na mbili, walikaidi. “Wakatoka nje, wakakimbia kutoka kaburini; kwa maana wameingiwa tetemeko na mshangao; wala hawakumwambia mtu neno, maana waliogopa” (16:8). Na kwa tukio hili, injili ya Marko inaishia hapo ghafla.[2]

**Yesu, Mwaminifu Pekee**

Mateso yalipokuja, marafiki wote wa karibu wa Yesu walishindwa; Ni Yesu tu aliyebaki mwaminifu. Hii inatufunza kitu fulani cha muhimu sana. Yesu pekee ndiye mwaminifu, na sisi tunabaki kuwa waaminifu kwa kunganishwa naye tu. Yesu aliishi maisha yake yote kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Katika ubatizo wake, mbingu zilifunguka na Roho Mtakatifu akaja juu yake Yesu katika umbo la njiwa. Katika kipindi chake cha huduma, Yesu mara nyingi alijitenga na makusanyiko ya watu ili kuwa na muda wa peke yake katika maombi, akimtegemea Mungu kwa nguvu na hekima. Yesu “alipotoa pumzi yake ya mwisho,” Roho Mtakatifu “akamtoka” (15:37). Na kwa hiyo, huo ukawa mwisho wa huduma yake yenye uwezesho wa Roho.

Kupitia nguvu za Roho mtakatifu, Yesu alitimiza kazi aliyopewa na Mungu kwa

uaminifu. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume, wanafunzi walipokea ujazo wa Roho. Kisha wakaanza kuponya wagonjwa, kutoa mapepo na kuwaongoza watu kwenye imani iokoayo. Peke yao, wanafunzi walishindwa vibaya mno. Kwa uwezesho wa Roho Mtakatifu, walifanya miujiza.

**Kumtegemea Aliye Mwaminfu**

Uanafunzi huanza pale tunapotambua kuwa Yesu ni Masihi, Mwana wa Mungu. Kama wale Kumi na mbili, tunakutana na mateso tunapomfuata Yesu. Ni lazima tubakie waaminifu zinapotokea fursa za kusimama na Yesu au kumkana tunapopitia mateso kuelekea utukufu.

Tunatazama, pengine, katika hali ya kukata tamaa, wanafunzi walipojikwaa na kuanguka. Ikiwa wao walishindwa, sisi twawezaje kuepukana na kushindwa? Twaweza pata wapi tumaini? Baada ya kufufuka kwa Yesu, wanafunzi walipokea Roho Mtakatifu. Matokeo yake, waligeuka na kuwa watu wa tofati kabisa walioleta injili kwa mataifa.

Wanafunzi waaminifu daima huelekeza macho yao kwa Yesu na kwa umuhimu kabisa wakiendelea katika kuungana naye.

C. S. Lewis alisema, “Mwana halisi wa Mungu yuko upande wako. Yuko anaanza kukugeuza uwe kitu fulani chenye kufanana na yeye mwenyewe.”[3] Tukiachwa wenyewe, tunashindwa. Lakini hatuko peke yetu. Tunao msaada wenyewe tunaouhitaji!

## Maswali kutoka Sura ya 3

1. Soma Marko 11:1-16:8. Weka kumbukumbu ya kila uchunguzi uonekanao kuwa wa muhimu. Una maswali gani?

2. Kiitikio mashuhuri chasema, "Nimeamua kumfuata Yesu, sitarudi, sitarudi. Hata wasipoenda nami, bado nitafuata." Mwishoni, wanafunzi wote walishindwa kumfuata Yesu.

   Lini ulishindwa kumfuata Yesu?
   Lini ulifanikiwa katika kumfuata Yesu?
   Unabakiaje katika kuungana na Yesu?

3. Roho Mtakatifu aliyatia nguvu maisha ya Yesu na huduma ili isianze kuisha kabla ya wakati wake. Kama tuonavyo wazi katika injili ya Marko, wanafunzi hushindwa pale wanapotumia nguvu zao wenyewe. Tunamtegemea Mungu kupitia maombi na kumruhusu Roho Mtakatifu kutenda kazi maishani mwetu. Elezea mafanikio yako ama kushindwa kwako katika kutegemea maombi na Roho Mtakatifu.

# Sura ya 4

## Ni nini Kifuatacho!
## Mawazo ya Kivitendo kuhusu Uanafunzi

Inatiaje hamasa kukutana na waongofu wapya kijijini kwako! Wewe ama mtu mwingine alionyesha mbegu za injili. Maisha mapya yakachochewa ndani ya mioyo yao. Kisha, kama vile mimea midogo, waongofu wapya wakaanza kuamini.

Katika Marko 4, Yesu anatoa simulizi kuhusu mkulima aliyekwenda nje kupanda mbegu. Baadhi ya mbegu zake ziliangukia kando ya njia. Ndege wakasema, "Asante sana," na wakafurahia chakula kizuri. Zingine zikaangukia penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara zikaota haraka kwa kuwa na udongo haba; hata jua lilipozuka ziliungua, na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka. Zingine zikaangukia penye miiba; ile miiba ikamea ikazizonga, zisizae matunda. Tofauti na zile zilizopandwa kwenye udongo wa kwenye miamba, mimea hii haikufa, lakini pia haikuzaa matunda. Mwisho magugu yaliingilia kati, yakiziharibu, na hazikuzaa matunda. Nini malengo ya ukulima? Kuzaa

matunda. Siyo tu kuotesha mimea, ila kuwa na mimea izaayo matunda.

Yesu aonyesha mlengo huu kwa kundi la mwisho la mbegu lililoangukia kwenye udongo mzuri. Zilikua katika uhai na zikazaa kwa wingi katika kiasi tofauti. Vivyo hivyo, tunapanda injili ili kuzaa *matunda* ya wafuasi wa Yesu, siyo tu waongofu wapya. Kwahiyo sasa nini kifuatacho kwa hawa watoto wapya waaminio waliokuja kijijini kwetu?

Katika injili ya Mathayo, Yesu analiacha kanisa kwa kazi ya *kufanya wanafunzi* (tazama Mathayo 28:19). Anasema tunafanya wanafunzi kwa kuwabatiza wale waaminio na kwa kuwafundisha kutii amri zote. Ubatizo, picha ya injili, inaruhusu wanafunzi kukiri imani yao katika Yesu hadharani. Katika kuzama majini, tunatambulika katika kifo chake. Ule utu wetu wa kale wa dhambi tuliokuwa nao umekufa na utu upya kama Yesu umekuwa hai. Kuibuka kutoka majini kunawakilisha shauku yetu ya kufanyika wanafunzi wa maisha yake na njia zake.

**Onyo kwa Waongofu Wapya**

Yesu hataki kuijaza mbingu na watu wenye kuomba sala ya toba na kuendelea katika njia

zao pasipo kubadilika. Kumbuka mwanzo wa kitabu hiki tuliongelea jinsi ambavyo Mungu alikusudia kuijaza dunia na watu wenye kufanana naye. Yesu atafanya kile ambacho Adamu wa kwanza alishindwa kufanya.

Ni lazima wanafunzi wataraajie upinzani. Kitu cha mwisho Shetani anataka, ni watu wenye kufanana na Yesu. Tangu siku ya kwanza Mungu alipoweka wanadamu duniani, adui amefanya jitihada za kuwafanya wanadamu wamfanane yeye na siyo Mungu. Shetani huwatia moyo watu kuukataa mpango wa Mungu na kuamua wao wenyewe nini ni chema na nini ni kiovu.

Kama shetani atashindwa kuwazuia watu kusikia na kuiamini injili, ataleta ugumu katika maisha yao. Ugumu unaweza kuharibu uzaaji wa matunda na hata imani yetu. Waongofu wapya, hasa wala wenye historia ya ibada za sanamu na roho, wanahitaji kuwa makini na ujanja wa Shetani.

Shetani yeye anataka tuione ibada kama siyo kitu kingine zaidi ya mpangilio wa biashara. Katika kitabu cha Ayubu, shetani anauliza, "Je! Huyo Ayubu yuamcha Bwana *bure*?" (1:9). Shetani hutulaghai katika kuwaza, "Hakuna ampendaye Mungu na kumtumikia

pasipo kupokea thawabu. Nikimfanyia bwana matendo mema, naye atanirudishia wema. Nawezaje kumfanya Mungu anipe kile nitakacho?" Maisha yakiwa magumu, mtu huyu anaweza kuwaza, "Pengine nimefanya jambo la kutompendeza Mungu." Huu ni moyo wa ibada za sanamu na roho: ikilaghai miungu or roho kunipatia kile ninachotaka au kuniepusha mbali na kile nisichokitaka. Cha kusikitisha, watu wengi wanaomkubali Kristo kamwe hawaikatii tamaa njia hii ya kumfikiria Mungu!

Watu wanaomtumaini Yesu wanahitaji kuelewa kwamba Ukristo sio tu "mkataba bora" kati ya "mikataba" mingine inayowezekana. Nyakati ngumu zitakuja. Maisha bado yataumiza vibaya wakati mwingine. Mungu mmoja wa kweli hawezi kudhibitiwa na mtu wa kawaida au mchawi. Mungu anatarajia sisi kumpenda na kumfuata hata ikiwa haileti maana au kutulipa kwa namna yoyote ndani ya muda mfupi. Mtu anapomgeukia Yesu, lazima tufunue njia hii ya uwongo ya kumkaribia Mungu na kuibadilisha na mafundisho ya Yesu.

Hata hivyo, Shetani hakatishwi tamaa kirahisirahisi. Kama hatafanikiwa kuharibu imani

ya muongofu mpya kwa kutumia ugumu, atatuma usumbufu kwa mtu huyu. Tunaweza kumuona akisema, "Acheni kanisa na lijenge majengo makubwa na liwe na mfumo mkubwa wa vyombo. Liwe na makongamano yenye kuwavuta watu wengi. Lifanye muziki wenye kuamsha hisia na kufanya watu wacheze sana. Lifanye matendo mema kama kuwalisha masikini. Lishughulike sana na miradi na programu, ilimradi tu halijishughulishi na uanafunzi!" Kitu Shetani hataki kuona ni dunia iliyojazwa na watu wenye kuishi na kupenda kama Yesu.

Yesu anataja "na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine" (Marko 4:19). Kuna watu wanataka zaidi ya kitu chochote kuonyesha miili yao mizuri na kuifunika na mavazi ya gharama kubwa. Wengine wanatoa kila kitu ili wapate elimu nzuri itakayowapelekea kuwa na kazi nzuri. Je, twaweza kusema mambo haya kuwa ni makosa? Hapana. Lakini yanaweza kutukosesha kuona yaliyo ya muhimu zaidi. Yanaweza kusababisha wasiwasi usio wa muhimu na kututaifisha nguvu za kumfuata Yesu.

Katika Somo la pale Mlimani, Yesu awaonya wanafunzi kutohofu juu ya mahitaji yao ya mwilini kama vile, wale nini, wanywe nini na wavae nini (Mathayo 6:25-34). Badala ya kuhofu twaweza kumwamini kwamaana Mungu huhusiana nasi kama vile baba kwa wanae. Anaahidi kutupa chochote kile tuombacho tunapoutafuta ufalme wake na haki yake kwanza maishani mwetu.

**Kugundua Zaidi kuhusu Yesu na Maisha yake**
Unatakiwa kuanzaje kuwafundisha waongofu wapya kuhusu kumfuata Yesu?

Ungeweza kuanza kwa kuwatembelea mara kwa mara. Anza kwa kusoma moja ya injili pamoja nao na familia zao. Mambo mazuri hutokea pale watu wanaposhikilia kioo cha neno la Mungu nyusoni mwao na pale wanaposhikilia upanga wa Roho mikononi mwao! Mambo muhimu hutokea kawaida unaposoma Biblia kidogo kidogo. Marko, injili fupi kuliko zote, ni mahali pazuri pa kuanzia. Usihofu kuhusu kumaliza eneo fulani la mnayoyasoma kila msomapo pamoja. Usihofu kuhusu kuandaa mambo mengi kabla ya wakati. Kwa urahisi kabisa soma kifungu na uulize maswali matatu marahisi:

- Najifunza nini kuhusu Mungu?
- Najifunza nini kuhusu njia mbaya wanazoziishi watu?
- Najifunza nini kuhusu jinsi gani mtu anatakiwa kuishi na kumfuata Yesu?

Chukua Marko 2:1-12 kama mfano. Yesu anamponya mtu aliyepooza baada ya wenzake kumpitisha katika tundu walilotengeneza kwenye paa. Tunajifunza nini kuhusu Mungu katika simulizi hii? Tunajifunza kwamba ni Mungu pekee anayesamehe dhambi. Yesu anadai kuwa na mamlaka ya kusamehe na anakazia madai yake kwa kufanya yale yasiyowezekana. Anamponya aliyepooza! Mungu pekee ndiye awazaye kuponya watu na kuwasamehe dhambi zao, kwahiyo ni lazima Yesu awe Mungu!

Naweza kujifunza nini kuhusu njia mbaya wanazoziishi watu katika simulizi hii? Wataalamu wa dini wa kiyahudi walimzushia Yesu ya kuwa amenena mabaya dhidi ya Mungu. Wakakataa ukweli ulio wazi ya kwamba Yesu ni Mungu. Anazo nguvu za kuponya na mamlaka ya kusamehe dhambi. Vivyo hivyo hata leo watu wanamkataa Yesu.

Najifunza nini kuhusu jinsi gani mtu anatakiwa kuishi na kumfuata Yesu katika simulizi hii? Tunapaswa kuamini ya kuwa Yesu ni Masihi. Alitumwa kutoka kwa Mungu na anaweza kutusamehe dhambi zetu. Kamwe hatupaswi kuipoteza ajabu hii na mshangao wetu juu ya mwanaume huyu wa ajabu aliyedhihirisha nguvu za Mungu hapa duniani.

Maswali mengine yataibuka kadri msomavyo Biblia pamoja. Ni sawa. Tena, ni nzuri sana! Ukiweza, wajibu, wakikujia. Ikiwa hujui jibu, weka wazi kwamba hujui na uwaambie kuwa utajaribu kutafuta jibu.

Mkiwa mnasoma Biblia pamoja, chagueni mistari ya kukariri. Mkikutana na mstari wa muhimu kama Marko 8:34b-35 katika usomaji wenu, kwanini msiukariri kwa pamoja? Yesu asema:

> Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili, huyu ataisalimisha.

Baada ya muda, kusoma na kukariri Biblia hubadilisha mawazo yetu.

**Sala**

Tunaonyesha uhitaji wetu wa Mungu kwa kumrudia tena na tena katika sala. Yesu alifanya mfano wa maombi kwa wanafunzi wakati wake wote hapa duniani. Hata wakati watu walipomdai mambo mengi, bado alitenga wakati wa kuomba. Bila shaka, Yesu alitumia muda fulani kuwaombea watu waliomfuata. Katika injili ya Luka, wanafunzi walimwendea Yesu na kumuuliza, "Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana [mbatizaji] alivyowafundisha wanafunzi wake" (Luka 11:1). Yesu aliwafundisha vitu vingi, lakini hususani kusali. Na kwa sababu ya hii, tunaweza kupata kile Yesu aliwafundisha katika kile tunachokiita "Sala ya Bwana" (mistari 2-4; pia, tazama Mathayo 6:9-13).

**Ushiriki wa Mikono**

Ufunguo katika uanafunzi ni uhusikaji. "Njoni mnifuate, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu!" Yesu aliwaita Simoni Petro na kaka yake Andrea (Marko 1:17). Walitii. Mwanzoni, walikuwa "pamoja naye" tu (Marko 3:14).

Lakini kadiri muda ulivyozidi kwenda mbele, Yesu aliwapa nafasi za kuponya wagonjwa na kutoa pepo. Wakati ungekuja ambapo angemrudia Mungu Baba, akiacha kazi hiyo kabisa mikononi mwao.

Unapotembelea watu kusoma Biblia au kushiriki injili, usiende peke yako. Nenda pamoja na mtu fulani. Wacha wakutazame ukifundisha, ukiomba na kuhudumia watu unaowatembelea. Wacha wahubiri, wasali, na kuhudumu pia.

Profesa wangu wa zamani aliwaambia wanafunzi wake, "Unaweza kuvutia kutoka mbali, lakini unaweza kuleta mguso ukiwa karibu tu." Ikiwa tunataka kweli kufanya wanafunzi, ni lazima turuhusu wafuasi wetu wakaribie vya kutosha kuona sisi ni kina nani na tunaishi vipi. Ni Lazima tupime nia zetu wenyewe. Je! Tunataka kukusanya umati wa mashabiki waliojitolea ambao watatoa pesa kwa kanisa? Au je! Tunatafuta kukuza watu zaidi ambao wanaonekana na kuishi kama Yesu, kuwashirikisha watu wengi katika jukumu la "kuvua watu"? Tunawawezesha wanafunzi kufanya wanafunzi zaidi pale tu tunapowaruhusu kushiriki katika huduma yetu. Lazima tuwapatie kazi za maana na mamlaka

(na labda hata kupiga makofi?) kwa wafuasi wetu. Tunapaswa kushiriki majukumu ya huduma pole pole, tukitoa majukumu makubwa tu baada ya wanafunzi kufanikiwa kumaliza madogo.

Mara kwa mara, wafanyao wanafunzi wanaweza kupata mgongano wa maadili. Miaka kadhaa iliyopita, nilitumikia kama mzee katika kanisa letu na mwalimu wa wahubiri wachanga katika chuo kikuu cha Biblia. Kanisa letu lilisema wazi maadili kadhaa, ikiwemo na "ibada inayochochea" na "kuwezesha uongozi." Mafundisho mazuri husaidia kufanya ibada iwe ya kutia moyo. Viongozi wanaowezesha kwa makusudi huwapa watu wadogo, wasio na uzoefu fursa, mafunzo, na mamlaka wanayohitaji kuongoza. Lakini tunaporuhusu watu wasio na uzoefu kuhubiri, ubora wa mahubiri mara nyingi hupungua kwa muda. Katika mgongano wa maadili kama huu, ni maadili yapi hushinda? Labda kwa kuweka hivi, ni nini muhimu zaidi? Je! Ungependa kuweka "onyesho" nzuri kila Jumapili au kukuza wanafunzi?

Tulimpa mwanafunzi mmoja anayeitwa Simon fursa ya kuhubiri. Alikuwa mzungumzaji mwenye kipawa na aliendelea

kukua. Leo anaongoza shirika la misheni la kimataifa huko Australia. Tuliwapa wanafunzi wengine nafasi za kuhudumu kwenye majukwaa madogo, kama vile kufanya kazi na vijana na kuongoza mafunzo ya kikundi kidogo cha Biblia.

Nelson na Van walichukua darasa langu la mbinu za kusoma Biblia katika mwaka wao wa kwanza katika chuo cha Biblia. Mwaka uliofuata walisafiri nami kwenda Ufilipino na walisaidia kuwafundisha waathirika wa madawa za kulevya walioanza kupona jinsi ya kujifunza Biblia. Katika mwaka wao wa tatu, walinisaidia kupanga upya maelezo kwa darasa la wiki saba juu ya jinsi ya kujifunza Biblia. Kisha tukafundisha darasa pamoja katika makanisa tofauti. Wote sasa wanahudumu katika makanisa yao wenyewe. Siku zote Yesu angeweza kufanya kazi bora peke yake kuliko kutumia wanadamu wenye kasoro, lakini alichagua kufundisha wengine na kutupitishia njia hii.

Wanafunzi wanahitaji "mafunzo" wanapojifunza kutumikia katika huduma. Vinginevyo, wanaweza kudhani wanajua vizuri wakati hawajui. Wanaweza pia kuvunjika moyo na kukata tamaa. Watoto

wengi wa Kitanzania wanapenda kucheza mpira. Mara nyingi tunawaona wakicheza na "mpira wa miguu" wa nyumbani na bila viatu. Ikiwa watashirikiana na kocha, baadhi ya watoto hawa watakomaa kadri mkufunzi wao anavyowafundisha juu ya mchezo huo, akiwaonyesha makosa yao kwa upole, akiwaonyesha njia bora za kucheza, na kuwafunza kimwili. Ndivyo ilivyo pia kwa uanafunzi. Wanafunzi wanahitaji "mkufunzi" anayeweza kuwafundisha juu ya huduma, kwa upole onyesha makosa yao, awaonyeshe njia bora za kutumika, na kuziamini.

**Muda na Uvumilivu**

Tunaposoma injili ya Marko, inatushtua kuona jinsi wanafunzi wa kwanza walivyokuwa taratibu na hata wenye vichwa vizito. Baada ya miaka mitatu, bado walishindwa kuelewa utume wa Yesu na nini maana ya kumfuata. Yesu alirudia mambo yale yale mara kwa mara, na hata wakati huo, ujumbe huo haukuzama ndani yao hadi hapo baadaye. Mwishowe, walishindwa kumfuata Yesu wakati alikuwa akiwahitaji zaidi.

Badala ya kuwakosoa wanaume hawa, wacha tuwatumie kama kioo ili tuone jinsi tuna-

vyoonekana. Na sisi tukiwa wakweli, tunajikuta pia tukichelewa kujifunza. Sisi pia tunajikwaa na kuanguka. Wale tunaotafuta kuwakuza kama wafuasi wa Yesu vivyo hivyo watajikwaa na kuanguka. Ukuaji huchukua muda. Kufanya wanafunzi kunahitaji uvumilivu. Lazima tukumbuke sio kila mtu anayeitikia injili anaendelea kuzaa matunda. Kumbuka mfano wa Mpanzi? Wengine huanguka wakati shida zinapokuja. Wengine hukengeushwa na tamaa za vitu vingine. Watu walianguka na kuvurugwa hata wakati Yesu alifundisha!

**We Ungefanya Nini?**

Ninajua kanisa ambalo linachukua ufuasi kwa umakini sana. Kila mwaka mchungaji huchukua kikundi kipya cha vijana kufundisha kwa miezi tisa. Wanakutana kila wiki kwa saa na nusu Jumanne, Jumatano, na Ijumaa asubuhi kuanzia saa 6:00 asubuhi. Pia hukutana pamoja kila Alhamisi usiku kwa masaa mawili. Kwa muda wa miezi tisa, wamekuwa wakisoma Biblia nzima na kujadili theolojia. Wanahudhuria pia mafungo manne ya wikendi mwaka mzima kusoma mada maalum kwa kina. Kwa miaka mingi,

wanaume mia kadhaa walimaliza programu na kuanza huduma.

Je Unaweza kuzingatia kitu kama hiki katika kanisa lako? Unaweza kuanza na wanaume au wanawake wachache tu, au labda hata mmoja tu mwanzoni. Bila kupuuza watu wengi wanaohitaji huduma ya kichungaji, je, unaweza kufikia hususani wachache ambao wanaonekana tayari kuchukua hatua kumfuata Yesu? Kwa uwezekano, tunaweza kukaa bize na kila aina ya shughuli kanisani, lakini Kristo alituamuru tufanye wanafunzi. Aliahidi kuwa atakuwa pamoja nasi njiani (tazama Mathayo 28: 18-20).

## Maswali kutoka Sura ya 4

1. Baada ya kusoma sura hii, unapaswa kufanya nini kifuatacho? Kwa kutumia maswali hapa chini fanya mpango wa kufundisha wengine kumfuata Yesu.

   - Anza na maombi. Omba Mungu akutangulie na akuongoze. Muombe akupe hekima na ujasiri na kuzaa matunda. Mshukuru kwa mavuno yajayo atakayoleta kupitia juhudi zako.

   - Je Kuna sehemu za kijiji chako ambapo unahitaji "kupanda mbegu zaidi"? Utakamilisha zoezi hili lini na wapi? Je Unaweza kwenda nani? Je Wewe na wale unaokwenda nao mnaweza kuelezea injili?

   - Je Ni waongofu gani wapya unahitaji kufuatilia? Je Wanahitaji kujua nini zaidi juu ya kumfuata Yesu? Tena, ni nani ungekwenda naye wakati unawatembelea waumini wapya?

2. Anza au endelea kusoma injili zingine mara kwa mara. Yesu alisema kufanya wanafunzi lazima tuwafundishe watu kutii amri zake zote (Mathayo 28: 28-20). Utafiti wa Mathayo unaonyesha mafundisho mengine matano muhimu kuhusu kumfuata Yesu.

   - Mahubiri ya Mlimani (Mathayo 5-7)
   - Kutumwa kwa wale Kumi na wawili (Mathayo 10)
   - Mifano ya Ufalme (Mathayo 13:1-52)
   - Maisha Kanisani (Mathayo 18)
   - Kufundisha juu ya Mlima wa Mizeituni juu ya Baadaye (Mathayo 24-25)

   Kila wakati unapojifunza, uliza maswali haya matatu juu ya kifungu hiki:

   - Ninajifunza nini kumhusu Mungu?
   - Ninajifunza nini juu ya njia mbaya watu wanaishi?
   - Je, ninajifunza nini juu ya jinsi mtu anapaswa kuishi na kumfuata Yesu?

# Hitimisho

Ikiwa umefikia hatua hii, labda una nia ya ufuasi. Tulianza kitabu hiki kwenye kochi lile kwenye chumba changu cha kulala miaka mingi iliyopita. Tangu wakati huo nimemwona Yesu—kwenye kurasa za injili, katika maisha ya washauri, katika sebule za washirika wa kanisa, katika washiriki wa familia, marafiki, wafanyikazi wenzangu, na hata mara kwa mara katika kielelezo kidogo katika kioo changu mwenyewe. Moja ya sababu kuu za Kanisa ni kuwafundisha watu kumfuata Yesu. Mungu atakaporudisha uumbaji katika siku zijazo, ulimwengu utajaa watu wanaofikiria, kutenda na kupenda kama Mungu mwenyewe.

> Baada ya mambo haya nilitazama, na tazama, umati mkubwa ambao hakuna mtu aliyeweza kuhesabu, kutoka mataifa yote na makabila na watu na lugha, wamesimama mbele ya kiti cha enzi na mbele ya Mwana-Kondoo, wakiwa wamevaa mavazi meupe na matawi ya

> mitende mikononi mwao. Wakalia kwa sauti kubwa wakisema, "Wokovu na uwe kwa Mungu wetu, kwa yule aketiye juu ya kiti cha enzi, na kwa Mwanakondoo!" (Ufunuo 7: 9-10)

Yesu aliwaita watu — mara nyingi waliochanganyikiwa na wenye kasoro kubwa — wamfuate. Lakini kwa uaminifu, je? Kuna aina nyingine yoyote. Baada ya muda, hawa watu wa kwanza ambao Yesu aliwaita walikuja kumtambua yeye ni nani. Walikubali utume wake, na mwishowe, wakamfuata, ingawa njia hiyo iliongoza kupitia mateso. Ikiwa haiwezekani kama inavyoonekana, mpango huo ulifanya kazi! Hapa tunakaa miaka elfu mbili baadaye. Ufalme wa Mungu huenea mbele yetu kama mmea mkubwa unaotoa kivuli kwa watu kutoka kila taifa, kabila, watu, na lugha. Kama chachu kwenye donge la unga, imefanya kazi sehemu kubwa ya dunia. Kama vile Yesu alivyotabiri, ufalme umekua.

Lakini kazi haijakamilika. Ikiwa ni hivyo, Yesu angekuwa amerudi kufikia sasa. Utume wetu unabaki pale pale—fanya wanafunzi. Njia inabaki ile ile—kubatiza na kufundisha watu kushika amri za Bwana. Wanafunzi

wenye uwezo hawaahidi zaidi au chini kuliko walivyowahi kuwa. Wengine wataacha. Wale ambao wanaendelea wataendelea kwa mwendo wa taratibu wenye maumivu. Lakini tunapoendelea na kazi hii ya wakati mwingine—kukatisha tamaa ya kufanya wanafunzi, Yesu alitupa kitiwa-moyo tunakohitaji. Baada ya kuwaamuru wanafunzi wake wafanye wanafunzi, Yesu aliwapa ahadi hii: "Hakika mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:20).

## Habari Njema kwako

Kitabu hiki kinatuhimiza kumfuata Yesu kwa kujifunza njia yake ya maisha. Kisha tunaweza kuonyesha wengine jinsi ya kumfuata pia. Tulijifunza pia jinsi dhambi inavyoharibu uhusiano wetu na Mungu na kutuzuia kumfuata Yesu. Kabla hatujaweza kumfuata Yesu, lazima tushughulike na dhambi zetu.

Suluhisho la shida yetu ya dhambi ni nini? Biblia inatuambia "Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka, wewe na nyumba yako" (Matendo 16:31). Hii inamaanisha nini hasa? Wacha tuchunguze Maandiko mengine ili kuelewa aya hii kikamilifu:

- Biblia inatufundisha kwamba hapo mwanzo Mungu aliumba ulimwengu mkamilifu ambao alitangaza kuwa "mzuri sana" (Mwanzo 1:1, 31).
- Wanadamu ambao Mungu aliwaumba na kuwaweka ulimwenguni hawakumtii. Wakati huo huo, dhambi iliingia ulimwenguni na kututenganisha na Mungu (Mwanzo 2:4-3:24).

- Mungu anatamani uhusiano na uumbaji wake na anapenda kila mmoja wetu. "Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).
- Kumjia Mungu, kwanza tunahitaji kutambua tunaishi mbali naye. "Kwa maana wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23).
- Hii ndio habari njema ya injili: Mungu alimtuma mwanawe Yesu afe msalabani na alipe gharama ya dhambi zetu. Alizikwa na kufufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu, akishinda kifo na dhambi. "Lakini Mungu anaonyesha upendo wake mwenyewe kwetu kwa hii: Tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo [Yesu] alikufa kwa ajili yetu" (Warumi 5:8).
- Tunaweza kukubali malipo ya dhambi zetu ambazo Yesu alifanya kwa ajili yetu. Tunaweza kumtumaini atuokoe kutoka kwa dhambi zetu na atuletee uhusiano na Mungu. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani - na hii haitokani na nyinyi, ni zawadi ya Mungu

- si kwa matendo, ili kwamba hakuna mtu anayeweza kujisifu" (Waefeso 2:8-9).

**Jinsi ya Kukubali Zawadi ya Wokovu:**

Sharti pekee la kupokea zawadi hii ni kuamini kweli hizi:

1. Mungu alituumba na anatupenda.
2. Kila mmoja wetu alizaliwa na dhambi na tunaendelea kutenda katika maisha yetu yote.
3. Yesu alikufa na kulipa gharama ya dhambi zetu.
4. Yesu, kupitia kifo na ufufuo wake, anatupatia zawadi ya msamaha.
5. Tunapoacha dhambi na kumgeukia Mungu kutuokoa, tunakuwa sehemu ya familia ya Mungu milele.

**Mfano wa Maombi ya Wokovu:**

Mungu Mpendwa, asante kwa kunipenda na kumtuma Mwana wako afe msalabani kwa ajili yangu. Natambua mimi ni mwenye dhambi na ninahitaji msamaha kwa dhambi zangu. Ninakubali malipo ya Mwanao kwa dhambi zangu msalabani. Asante kwamba Yesu

alishinda kifo na akafufuka kutoka kwa wafu. Asante kwa kunikubali katika familia yako na kunipa maisha na wewe milele. Tafadhali nisaidie kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu wakati ninaishi hapa duniani.

# Maelezo ya mwisho

1 Kitabu hiki kitafuata muhtasari huu kwa kumtazama Marko. Ufafanuzi wa msomi wa Biblia Abraham Kuruvilla, *Marko: Ufafanuzi wa kitheolojia kwa Wahubiri* umekuwa msaada kwa kuelewa muundo wa Marko.
2 Wanafunzi wengi huiona mistari 9-20 kama ongezeko la baadaye la toleo fupi la kwanza la Marko.
3 CS Lewis, *Ukristo wa Kawaida* (New York City: Harper Collins, 1952), toleo la Kindle.